

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1

Nukushi: 255-262961502

Barua pepe : press@ikulu.go.tz

Tovuti : www.ikulu.go.tz



*OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS
NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.*

*Morogoro
03 Agosti, 2024*

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema ni jukumu la Serikali kulinda na kutetea maslahi ya makundi yote katika jamii hivyo itaendelea kusimamia maslahi ya wananchi wanaotaka sukari ya uhakika kwa bei himilivu.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo wakati wa uzinduzi wa Bwawa la Umwagiliaji la Kiwanda cha Sukari Mtibwa, Morogoro, ambao unaenda kuongeza uwezo wa kiwanda hicho kuzalisha sukari.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema Serikali inatambua umuhimu wa viwanda vya sukari nchini na ina dhamira ya kuvifanya viimarike, viongeze tija na uzalishaji ili viweze kunufaika na soko la ndani lililopo, na kuiwezesha nchi kujitosheleza kwenye uzalishaji wa sukari.

Akiwa Wilaya ya Mvomero, Rais Dkt. Samia amezindua kampeni ya TUTUNZANE yenye lengo la kutunza amani na kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Rais Dkt. Samia amepongeza ari ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mkoa na Wilaya kwa kutatua changamoto kwa ubunifu na kutafuta suluhu za kudumu kwa matatizo yanayowakabili wananchi.

Rais Dkt. Samia pia amesisitiza kuwa dhamira ya Serikali ni kuongeza nguvu katika kutatua matatizo yanayohusu matumizi ya ardhi, ikiwemo migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Hali kadhalika, Rais Samia pia ametembelea Kiwanda cha Mbegu (ASA) na kujionea uzalishaji na utunzwaji wa mbegu za asili nchini, na amewataka wawe wabunifu zaidi na kuendelea kuzalisha mbegu bora ili kuongeza tija kwenye kilimo nchini.

Kwa upande mwingine, Rais Samia amezindua rasmi barabara ya Rudewa - Kilosa yenye urefu wa kilomita 25 iliyokamilika kwa kiwango cha lami. Rais Dkt. Samia amewahakikishia wananchi kuwa Serikali itakamilisha mradi wa Dumila-Kilosa-Ulaya-Mikumi yenye urefu wa kilomita 142 ambayo itachochea maendeleo wa maeneo hayo na kuongeza fursa za ajira na kipato kwa wananchi.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Sharifa B. Nyanga'.

Sharifa B. Nyanga

Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

